

# SIMULIZI ZA MABADILIKO

## The Story of Change



ELIMU YA USAWA  
WA JINSIA  
YAONGEZA  
USHIRIKI WA  
MTOTO WA KIKE  
MASOMONI



Mpwapwa Dc

# SIMULIZI YA MABADILIKO

## Usawa wa Jinsia

“Samaki Mkunje angali Mbichi” ni maneno ya wahenga yanayodokeza uwepo wa jambo. Usawa wa Kijinsia si jambo geni msisitizo wake umekuwa na msambao popote Ulimwenguni ambapo wanaharakati mbali mbali wameweka nguvu nyingi katika kuhamasisha suala zima la uwepo wa usawa baina ya mtoto wa kike katika masuala mbali mbali likiwepo suala la Haki Sawa ya kupata elimu kwa watoto wa kike na kiume.

Katika kuhakikisha kuwa Dhana hii ya usawa wa jinsia inaeleweka kwa watoto tangu wakiwa wadogo ili wakue nayo katika makuzi, Mgoma kuna chakujifunza.

# Usawa wa Jinsia

- ▶ Mwal. Bahati Mgwambusa ni mwalimu wa Darasa la pili katika Shule ya msingi Mgoma, shule iliyopo kata ya Godegode Wilayani Mpwapwa. Mwalimu anatanabaisha mbinu mbalimbali anazozitumia katika kufundisha masuala ya Usawa na Jinsia kwa wanafunzi shuleni Mgoma. Katika shule hii kuna Baraza la shule ambalo hukaa kila mwisho wa mwezi ambapo walimu na wanafunzi huwa na mjadala wa mada ya Usawa wa jinsia huku wakiongozwa na Picha zilizochorwa kusadifu Mada sanjari na simulizi za hadithi na maigizo.

# Simulizi za Mabadiliko (SMZ)

*“Sote tushirikiane Kujifunza, Majukumu ya Nyumbani ni ya kwetu Sote”*

Katika Picha hizi Picha ya kwanza inaonesha ushirikiano wa mtoto wa kike na kiume katika kusoma kitabu na kujadiliana kwa pamoja darasani, Huku picha ya Pili ikionesha namna mtoto wa Kike na Kiume wanavoshirikiana katika kufanya shughuli za Nyumbani wakitoka shuleni.



Mojawapo ya Picha zilichorwa katika Mbao za matangazo kwaajili ya Mjadala wa Mada ya Usawa wa Jinsia Katika Baraza.

# Matokeo ya Elimu ya Usawa wa Jinsia

▶ Mwal.Mwambusa anaelezakuwa ujifunzaji huu wa Masuala ya Usawa wa Jinsia umekuwa na matokeo chanya.;

- ▶ Ufafanuzi wa picha Wanajifunza kwa Pamoja
- ▶ Nidhamu imeongezeka
- ▶ Watoto Wa Kike Wameongeza Ushiriki wa Kuuliza maswali darasani kama watoto wa kiume
- ▶ Watoto wa Kike wamekuwa Wakijiamini zaidi
- ▶ Watoto wa Kiume wamekuwa Mstari wa mbele kufanya kazi Za Nyumbani wakisaidiana na watoto wa Kike.



# SIMULIZI ZA MABADILIKO

Asanteni Kwa Kufuatilia Simulizi hii



▶ Waandazi

▶ Beyond Samwel Madege 0717055707

▶ Juma Butie  
▶ Anderson Njolegwa  
▶ Alexander Kiowi